JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO

# Sauti ya
## Manispaa ya Morogoro



17



04



09




20



# Jarida la Mwezi

## Mwezi Oktoba 2022

## Toleo namba 08



# BODI YA UHARIRI

**Mhariri Mkuu ...** **Lilian K. Henerico**
*Afisa Habari Manispaa*

## Washiriki wasaidizi

**Neema Mwambi:** *Afisa Habari Msaidizi*

**Issa B. Issa:** *Afisa Habari Msaidizi*

**Yusuph A. Mwamba**
*Afisa Habari Msaidizi*

*mawasiliano:* *simu: 023 - 2935242*
*E-mail: info@morogoromc.go.tz*
*S.L.P 166*

*Mitandao ya Kijamii*

| | |
|---|---|
| *Website:* | *www.morogoromc.go.tz* |
| *youtube:* | *Moromc online tv* |
| *instagram:* | *Manispaa ya Morogoro* |
| *facebook:* | *Manispaa ya Morogoro* |



MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Fatma Mwassa (wapili kutoka kulia) akikagua kitabu cha wageni katika ziara zake za kukagua miradi ya Maendeleo Manispaa ya Morogoro.

# RC Mwassa aridhishwa na utekelezaji wa Miradi Manispaa ya Morogoro.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Fatma Mwassa, amefanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika Manispaa ya Morogoro lengo ikiwa ni kuangalia namna miradi hiyo inatekelezwa huku akielezea namna ambavyo amefurahishwa na utekelezaji wa miradi hiyo.

Akiongea katika ziara hiyo RC Mwassa, ameipongeza Manispaa ya Morogoro, kwa utekelezaji wa miradi hiyo na kwa jinsi wanavyoshirikiana vyema baina ya viongozi wa Serikali na wa chama katika kuhakikisha miradi ya maendeleo inatekelezwa ipaswavyo.

Aidha RC Mwassa, alisema ofisi yake itafanyia kazi maoni ya wananchi pamoja na viongozi ikiwa ni lengo la kuufanya Mkoa wa Morogoro kuwa na maendeleo makubwa .

RC Mwasa, alisema amefurahishwa na ushirikiano alioupata wakati wa ukaguzi wa miradi hiyo na amewataka watumishi wa Serikali na viongozi wote wa Manispaa kuendelea kushirikiana na kuwasisitiza kusimamia vyema ukusanyaji wa mapato.
Pia RC Mwassa, amesisitiza viongozi wote wa Manispaa kufanya ufuatiliaji wa shughuli za miradi, kusikiliza na kutatua kero za wananchi, kuendelea kusimamia usafi wa mazingira, kuendelea kuyalinda maeneo ambayo machinga wameondolewa.

Nae Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Albert Msando, amemshukuru Mkuu wa Mkoa kwa ziara yake na kuahidi kuwa maelekezo yote aliyoyatoa yatafanyiwa kazi na kutekelezwa ipaswavyo na kuhakikisha Wilaya ya Morogoro inaendelea kuwa ya mfano kwa nyanja zote.

Katika ziara hiyo iliyofanyika Septemba 12/2022, RC Mwasa, ametembelea mradi wa Ujenzi wa Shule Mpya ya ghorofa iliyopo Kata ya Boma, Ujenzi wa Kituo kipya cha Afya Kata ya Tungi, Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, mradi wa Pampu ya Maji Kihonda Mizani, Ujenzi wa Kituo kipya cha Afya Lukobe, Shule mpya ya Sekondari Lukobe pamoja na Shule mpya ya Sekondari ya Mindu.



Picha mbalimbali zikionesha matukio tofauti tofauti ya Ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Fatma Mwassa za kukagua ujenzi wa Miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Manispaa ya Morogoro














Mstahiki Meya Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga (wapili kutoka kulia) akikata utepe kuashiria uzinduzi wa madawati 200 yaliyotengenezwa na Baraza la Maendeleo la Kata ya Kilakala (wapili kushoto) Katibu wa CCM Wilaya ya Morogoro Mjini, Chifu Sylevester Yared (watatu kushoto) Diwani wa Kata ya Kilakala , Mhe. Marco Kanga.

# MEYA KIHANGA AKABIDHI MADAWATI 200 KATA YA KILAKALA.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, amekabidhi madawati 200 yaliyogharimu Milioni 2 na laki 6 kwa shule 3 za Msingi ikiwamo shule ya Mwande, Kigurunyembe na Kilakala yaliyotengenezwa kupitia uvunaji wa rasilimali ya miti chini ya usimamizi wa Baraza la Maendeleo la Kata ya Kilakala.

Akizungumza wakati wa kukabidhi madawati hayo, Mhe. Kihanga, ameupongeza Uongozi wa Kata ya Kilakala chini ya Diwani Mhe. Marco Kanga pamoja na wadau wote waliofanikisha utengenezaji wa madawati hayo.

Mhe. Kihanga, amewataka wakuu wa shule hizo 3 ambao wamekabidhiwa madawati hayo kuhakikisha madawati hayo yanatunzwa vizuri ili yaweze kudumu kwa muda mrefu na kutumiwa na wanafunzi wengine hapo baadaye.

Kwa upande wa Katibu wa CCM Wilaya ya Morogoro Mjini, Chifu Sylvester Yared, ameupongeza Uongozi wa Kata kwa hatua ya kuboresha elimu huku akisisitiza kusimamia elimu kwani kipaumbele ni taaluma inayoweza kuleta mapinduzi makubwa katika sekta ya elimu katika Taifa letu ambapo amesema Serikali ya awamu ya Sita inafanya jitihada kubwa katika suala la kuboresha elimu kwa kujenga miundombinu mbalimbali.

Naye Diwani wa Kata ya Kilakala, Mhe. Marco Kanga, alisema Shule za Msingi Kata ya Kilakala zilikuwa zinakabiliwa na uhaba wa madawati hivyo anaamini madawati hayo yatakidhi haja na kuondoa tatizo hilo. " Nawashakuru wadau wote waliofanikisha utengenezaji wa madawati haya, tunamshukuru Mkuu wetu wa Wilaya kwa ushirikiano wake , Mkurugenzi wa Manispaa, Mbunge wetu Mhe. Abood na wadau wote pamoja na waalimu waliojitolea fedha katika kufanikisha hili, sasa tunahamia katika shule za Sekondari ili tumalize sasa matatizo ya madawati katika shule zetu za Msingi na Sekondari" Alisema Mhe. Kanga.




Madawati  yaliyotengenezwa na Baraza la Maendeleo la Kata ya Kilakala kwa kushirikiana na wananchi na wadau.








# HABARI PICHA KUONESHA MUONEKANO WA HOSPITALI YA WILAYA YA MOROGORO









# Jenista awapongeza wanufaika wa TASAF Manispaa ya Morogoro kwa kuanzisha Miradi yenye tija kujipatia kipato.




WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama ameridhishwa na walengwa wa Mpango wa Kuzinusuru Kaya Maskini Manispaa ya Morogoro kwa kuendesha mradi wa funza chuma kwa ajili ya kuzalisha chakula cha mifugo kinachowaongezea kipato na kutatua changamoto ya upatikanaji wa chakula cha mifugo.

Jenista alisema hayo, baada ya kukagua mradi wa kuzalisha funza chuma, unaotekelezwa na walengwa wa TASAF wa kikundi cha Faraja kilichopo mtaa wa Mazimbu Darajani , Kata ya Mazimbu, Manispaa ya Morogoro.

Mpango huo wa Kuzinusuru Kaya Maskini sehemu ya pili unaoratibiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

Alisema kumekuwa na shida ya upatikanaji wa chakula cha mifugo hivyo mradi huo unaotumia teknolojia rahisi kuzalisha funza chuma kwa ajili ya chakula cha mifugo utatatua changamoto ya upatikanaji wa chakula cha mifugo wakiwemo ng'ombe, kuku na Samaki.

"Mmesema hapa kupitia taarifa yenu kuwa, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimefanya utafiti na kubaini kuwa funza chuma ni chakula kizuri cha mifugo kuliko vyakula vingine ambavyo vimekuwa vikitumika kulisha mifugo na mradi huu ni mzuri na wa kimkakati ambao unapaswa kuendelezwa,"alisema Jenista

Alisema mradi huo utasaidia kuhifadhi mazingira na kutatua changamoto ya uchafu wa mazingira katika masoko kwani badala ya taka kutupwa hovyo ndani ya masoko, zitachukuliwa ili kuzalisha chakula cha mifugo na kuacha masoko yakiwa kwenye hali ya usafi.

"Huu mradi ni suluhisho kubwa la changamoto ya uchumi, uchafu wa mazingira na suala la ajira kwa makundi yote ya akina mama, vijana na wenye ulemavu na walengwa wa TASAF, kwani ni mradi fungamanishi wenye faida nyingi,"alifafanua Jenista

Naye Meya wa Manispaa ya Morogoro,Pascal Kihanga alisema mradi wa funza chuma una faida kubwa katika jamii, kwani utasaidia Manispaa kuwa na mazingira safi na kuboresha maisha ya wananchi kwa kuwaongezea kipato.

"Kutokana na faida ya uwepo wa mradi huu, Manispaa ya Morogoro itawatumia Wahandisi waliopo kuwajengea walengwa wa TASAF na wananchi wengine vizimba vya kufuga funza chuma ili waweze kuzalisha kwa wingi chakula cha mifugo ambacho kitawaongezea kipato chao " alisema Kihanga.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Manispaa  Ally Machela alisema katika mwaka wa fedha wa Julai , 2021 hadi Juni , 2022 , Manispaa ilipokea jumla ya Sh milioni 904.2 .

Alisema fedha taslimu zilizolipwa kwa walengwa kwa njia ya mtandao na benki ni Sh milioni 390.9 ambazo zililipwa kwenye namba za simu na akaunti za benki za walengwa moja kwa moja.

" Manispaa kupitia mpango huu inaendelea kutoa elimu kwa walengwa juu ya matumizi sahihi ya fedha na kuwahimiza kutoa taarifa , kuanzia viongozi wao wa Serikai za mitaa mara anapohama na kuripiwa katika Serikali ya mtaa wanapohamia " alisema Machela.

Nao baadhi ya wanufaika na mpango huo kwa nyakati tofauti waliishukuru Serikali kupitia TASAF kuwawezesha kifedha ambazo wamezitumia kusomesha watoto wao ,kuanzisha miradi midogo ya uzalishaji mali iliyowezesha kuwa na makazi bora.



# RC MWASA AWATAKA VIONGOZI KUTATUA KERO ZA WANANCHI.



Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Fatma Mwasa, amewaagiza Viongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kufanya ziara za kusikiliza kero za wananchi na kuzipatia ufumbuzi badala ya kusubiri viongozi wa Serikali ya mkoa ndio wazitatue changamoto za wananchi.

Ametoa agizo hilo wakati wa Mkutano wa hadhara wa kusikiliza na kutatua kero za Wananchi Kata ya Kihonda, uliofanyika Septemba 13/2022 katika eneo la Ofisi ya Kata ya Kihonda .

RC Mwasa, alisema Serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo lakini wananchi hawajui kinachoendelea kwasababu viongozi ambao wanapaswa kuwaeleza hawafanyi hivyo.

"Ni muhimu mno kufanya mikutano ya wananchi kusikiliza kero zao, wahamasisheni Madiwani, Makatibu Tarafa wafanye ziara, mkoa wetu umekuwa ukipata fedha nyingi za miradi ya maendeleo ni wajibu wetu kama viongozi kuzisimamia ili zilete tija katika maendeleo," Amesema RC Mwassa.

Aidha, alisema kuwa kusikiliza ni moja ya uwajibikaji bora kwa wananchi, hivyo kutofanya mikutano ya hadhara kwa wananchi kunasababisha kuibuka kwa kero nyingi ambazo kama ziara zingekuwa zinafanyika hali hiyo isingejitokeza.

Katika hatua nyingine, amepiga marufuku Watendaji wa Kata na Mitaa na wenyeviti wa Serikali za Mitaa kutojihusisha na uuzaji wa ardhi, kwani kufanya hivyo kuna pelekea kuwa na mlundikano wa migogoro ya ardhi kilasiku.

Hata hivyo, RC Mwasa, amewaagiza Viongozi wa Wilaya na Halmashauri kwa kushirikiana na wataalam wa ardhi kufuatilia migogoro yote ya ardhi na kuipatia ufumbuzi na kuiweka kwenye "data base".

Kwa upande wake Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Dkt. Mussa Ali Mussa, amemuhakikishia Mkuu wa Mkoa kuwa yote aliyoyaagiza atayafanyia kazi kwa kushirikiana na Watendaji wa Halmashauri zote za Mkoa huu.

RAS Mussa, amewataka Watumishi wa Umma kuhakikisha kila mtumishi awe na sheria ya Serikali za Mitaa ambayo sheria hiyo ndio inayoonesha majukumu yao kwa ujumla katika kuwatumikia wananchi.

"Mkasome sheria za Serikali za Mitaa, lakini kila mtumishi awe na Ilani ya CCM inayoelekeza mambo ya kufanya , pia tuangalie maelekezo ya mkoa yanataka nini , tujenge utamaduni wa kuwajibishana ili mifumo ifanye kazi , kwa kufanya haya tunaamini kabisa tutaweza kufikia viwango vya juu vya utendaji " Amesema RAS Mussa.



MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Fatma Mwassa,akizungumza na wananchi wa Kata ya Kihonda katika Mkutano wake wa kusikiliza na kutatua kero za wananchi uliofanyika Septemba 13/2022.








MSTAHIKI Meya Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, akiwa pamoja na watu wenye Ualbino Manispaa ya Morogoro waliopewa fedha za mitaji na Taasisi ya ADRA Tanzania katika Ukumbi wa DDC Mbaraka Mwishehe Manispaa ya Morogoro.

# Meya Kihanga atoa neno kwa watu wenye ualbino waliopatiwa Mitaji.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, amewataka watu wenye Ualbino 19 waliopatiwa mitaji kuhakikisha wanatumia mitaji hiyo kwa kutekeleza malengo waliyojiwekea.

Kauli hiyo,ameitoa, Septemba 6/2022 wakati wa hafla fupi ya utoaji wa ruzuku kwa watu wenye Ualbino kupitia ufadhili wa ADRA Tanzania katika Ukumbi wa Mbaraka Mwinshehe Manispaa ya Morogoro.

" Ninawaomba sana mitaji hii mliyopewa mkaitumie kwa malengo mliyojiwekea,kuna baadhi ya watu wanatabia wanapopewa mitaji au mikopo hii ubadiri mawazo na malengo yao na kuamua kuzigawana fedha kwa matumizi binafsi,kumbukeni wafadhili wetu wametoa fedha na ni matarajio yao kuona fedha hizi zinazaa matunda, lakini niwaombe mkajiunge vikundi Manispaa inatoa asilimia 10 ya mapato ya ndani kama mkopo ili kuwawezesha wananchi kujikwamua kiuchumi, Imani yangu mtafanya vizuri kwa kuwa tayari nimesikia mshapata mafunzo ya namna ya kuendesha biashara zenu" Alisema Mhe. Kihanga.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa ADRA Tanzania, Sam Oyortey, alisema bado kuna kundi kubwa la watu wenye ulemavu wanaopaswa kuwezeshwa ujuzi na mitaji ili waweze kujitafutia kipato. Oyortey, ameiomba Manispaa ya Morogoro licha ya walemavu hao kupatiwa mitaji lakini Manispaa ijikite katika kuona namna ya kuwaongezea mitaji katika mikopo yao ya asilimia 2.

Naye Mwenyekiti wa Watu wenye Ualbino Mkoa wa Morogoro Hassan Mikazi, alisema kukosekana kwa mitaji kwa watu wenye ulemavu umesababisha wengi wao wanakosa fursa mbalimbali ambazo zingeweza kupunguza viwango vya umasikini.






Wanafunzi wakiwa katika maandamano ya Maadhmisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika Duniani ambapo kwa Manispaa ya Morogoro yalifanyika katika Viwanja vya Shule ya Msingi Mwembesongo Kata ya Mji Mpya Juni 16/2022.










MSTAHIKI Meya Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, akizungumza na wananchi katika Maadhmisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika Duniani ambapo kwa Manispaa ya Morogoro yalifanyika katika Viwanja vya Shule ya Msingi Mwembesongo Kata ya Mji Mpya Juni 16/2022.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Albert Msando, akionesha mchoro wa ramani wa eneo la Star City Kiegea, (kushoto),Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Ally Machela.



# DC MSANDO AKABIDHI MCHORO WA KIMKAKATI KWA WANANCHI WA STAR CITY KIEGEA




Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Albert Msando, amekabidhi mchoro wa kimkakati wenye lengo la kuujenga Mji wa Kiegea A na B eneo la Star City Manispaa ya Morogoro.
Mchoro huo amekabidhi Julai 14/2022 katika mkutano wake na wananchi wa eneo hilo ikiwa ni maandalizi ya kuupanga mji huo.

Akizungumza na Wananchi hao, DC Msando,alisema kuwa Wananchi wa Star City watembee kifua mbele kwani wanakwenda kumiliki ardhi yao waliyokuwa wakiisubiria kwa muda mrefu kufuatia eneo hilo kuwa na sintofahamu na mwekezaji.
Pamoja na kukabidhi ramani hiyo, DC Msando, alisema mji huo wameupanga na kuwa mji wenye hadhi ya kipekee ambao utakuwa na huduma zote muhimu za kijamii na kufungua fursa za ajira kwa wananchi wa eneo hilo.

“Tumewaletea huu mchoro, tulianza na upimaji tukiwa na lengo la kila mwananchi aliye na kipande cha Ardhi anakuwa na hati yake miliki ili kujiletea maendeleo, niwaombe baada ya kumiliki haya maeneo msiyauze ,yatunzeni kwa ajili ya vizazi vyenu vya baadae ardhi ni hazina, hata mjini nako kulikuwa kama hivi” Alisema DC Msando.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Ally Machela, alisema kwa sasa hatua iliyofikia ni kuhakikisha mji huo unachongwa barabara zote kabla hawajatoa maelekezo ya ujenzi wa nyumba kufuatia kukabidhiwa ramani hiyo.
Machela, alisema kwa sasa Mji unahitaji kupangwa hivyo wananchi lazima wasikilize maelekezo na maagizo ya viongozi badala ya kukiuka maagizo hayo.
Naye , Afisa Mipango Miji Manispaa ya Morogoro, Emeline Kihunrwa, alisema kwa sasa timu ipo kazini kuhakikisha eneo hilo lote lenye ekari 4500 linapimwa na kupangwa ili wananchi waweze kupata hati zao.
Upande wa Mwananchi, Elizabeth Chigua, aliushukuru Uongozi wa Mkoa, Wilaya na Manispaa kwa kuchukua hatua za kuwatambua na kuwamilikisha ardhi baada ya muda mrefu kuitwa wavamizi.





DIWANI wa Kata ya Kihonda, Mhe. Hamisi Kilongo ,akizungumza na wananchi wa eneo la Star City katika mkutano wa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro ya kuonesha mchoro wa mji wao unavyotakiwa kupangwa.









Matukio mbalimbali katika picha ya Ziara ya Mkuu wa Wilaya ya MorogoroMhe. Albert Msando ya kusikiliza na kutatua kero za wananchi wa Kiegea A&B(Star City)



# Manispaa ya Morogoro yaendelea kutoa Matibabu bure kwa Wazee.


Katibu wa Afya Manispaa ya Morogoro Bertha Mahanga, (kushoto) akitoa kitambulisho cha matibabu bure kwa Wazee wa Makao ya Fungafunga yaliyopo Manispaa ya Morogoro,(wapili kutoka kulia) ,Mratibu wa Wazee Manispaa ya Morogoro, Rehema Malimi.

Manispaa ya Morogoro itaendelea kusimamia utoaji wa matibabu kwa Wazee bila malipo, upatikanaji wa dawa Hospitalini na uwepo wa dirisha maalum kwa ajili ya Wazee ili kuwaenzi na kuwaondolea usumbufu.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Katibu wa Afya Manispaa ya Morogoro Bertha Mahanga ,akimwakilisha Mganga Mkuu wa Manispaa ya Morogoro kwa niaba ya Mkurugenzi wakati wa kugawa vitambulisho katika Makao ya Wazee Fungafunga Kata ya Kichangani.

Aidha, Mahanga , amesema Manispaa ya Morogoro , itaendelea kutoa huduma kwa wazee pasipo kuchangia gharama za matibabu na kuboresha changamoto ambazo zimejitokeza katika utoaji wa huduma hiyo kwa kundi hilo.

"Sisi sote ni mashahidi wa utolewaji wa huduma za Afya bila malipo kwa Wazee wote,nitoe wito kwenu kufika kwenye vituo vya huduma za Afya vya Serikali ili kupatiwa huduma bila kuchangia gharama za matibabu"Amesema Mahanga.

Kwa upande wa Afisa Ustawi wa Jamii na Mratibu wa Wazee Manispaa ya Morogoro, Rehema Malimi, amewaomba Maafisa maendeleo ya jamii wa kila Kata kuwashauri wazazi ambao watoto wao wanalelewa na wazee kuona umuhimu wa mtoto kuishi na mzazi ili kuwapunguzia majukumu.

Aidha,amesema Malezi ya watoto hao ni jukumu la wazazi wao hivyo ni vema tukawaelimisha watoto na wajukuu zetu juu ya umuhimu wa malezi ya Wazazi kwa watoto.

"Kwa kuwa kila Kata kuna Maafisa Ustawi wa Jamii niwaombe mfike ili wazazi hawa waweze kuwajibika kama Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009 inavyoelekeza".Amesema Malimi.

Mwisho, Malimi, amempongeza Rais Samia kwa kazi nzuri ya kusimamia huduma za afya hususani katika kuwajali Wazee katika suala zima la matibabu bure na kutoa shukrani kwa viongozi wa Baraza la Wazee Manispaa ya Morogoro kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuwaunganisha Wazee katika kuhakikisha wanapatiwa mahitaji yao ya Msingi.

Naye Mwenyekiti wa Wazee Fungafunga, Mzee Joseph Kaniki, ameushukuru Uongozi wa Manispaa ya Morogoro kwa kutekeleza ugawaji wa Vitambulisho pamoja na hatua wanazoendelea kuzichukua katika kuimarisha Sekta ya afya hasa kwa wazee.
Hivyo, Mzee Kaniki, amezidi kuchukua nafasi ya kumuombea Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan afya njema ili aweze kuiongoza vyema Tanzania katika kufikia maendeleo.

Katika utoaji wa Vitambulisho kwa Wazee wa Fungafunga, jumla ya Wazee 21 wamepigwa picha bure na kukabidhiwa Vitambulisho vyao vya msamaha wa matibabu.

# MAPATO YA NDANI BILIONI 1.2 MANISPAA YA MOROGORO YANATUMIKA KUJENGA KITUO CHA AFYA KATA YA TUNGI.

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa mara ya kwanza tangu ilipoanzishwa inatekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa Kituo cha kisasa cha Afya Tungi kitakachogharimu kiasi cha Sh bilioni 1.2 , fedha zinazotokana na mapato yake ya ndani.
Kituo hicho cha afya kitakachokuwa na huduma zote muhimu za afya kitahudumia watu takribani 16,793 wanaoishi Kata ya Tungi na nyingine za jirani katika Manispaa ya Morogoro .

Mkurugenzi wa Manispaa Ndg. Ally Machela amesema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea kujionea shughuli za ujenzi wa kituo hicho eneo la kata ya Tungi.

Machela alisema kituo hicho kinajengwa kwa kufuata maelekezo ya Wizara ya Afya na kina majengo 10 ya kutolea huduma mbalimbali kwa wananchi na kwa hatua ya kwanza ujenzi wake umetumia Sh milioni 350 ,fedha zinazotokana na makusanyo ya mapato ya ndani.

"Kwa sasa tupo katika hatua ya upauaji na tayari tumelipa fedha Tsh Milioni 83 za ununuaji wa bati na bati hizo wametuahidi wiki ijayo kiwanda kitaleta hizo bati " amesema Machela
Alisema mradi huo wa ujenzi katika kata ya Tungi umekuwa ni ukombozi mkubwa kwa wananchi wake na wengine wa kata za jirani kupata huduma za afya eneo la karibu .

“ Malengo ya Manispaa yalikuwa ni kujenga kituo cha afya ambacho kimetimia na kwa ujumla tumekidhi vigezo vyote vya majengo yote yanayotakiwa kwa ajili ya mradi wa afya” alisema Machela.

Mkurugenzi wa Manispaa alisema uamuzi huo ni kwa ajili ya kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha ya kwamba huduma za afya zinafanyika katika kiwango ambacho ni timilifu kwa upatikanaji wa huduma zote muhimu kwa asilimia 100.



“ Ujenzi huu unafanyika kwa fedha za mapato ya ndani ,na Manispaa imeamua kwa makusudi kuhakikisha ya kwamba tuna kuwa na mradi mkubwa unaotokana na mapato ya ndani tuna miradi mingi ya mapato ya ndani lakini huu ni mahususi kwa ajili ya kituo cha afya na mahususi katika sekta ya afya “ alisema Machela
Machela alisema majengo hayo yatawekewa njia maalumu za kupita wagonjwa na watoaji wa huduma katika Kituo hicho .
Machela pia alisema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 , Halmashauri imetenga fedha za kumalizia Zahanati nne zilizopo kata ya Kingo , Kauzeni, Mkundi na Mazimbu na ndani ya miaka miwili , Manispaa itakuwa na zahanati zaidi ya 10 zilizokamilika na zinazotoa huduma.

Naye Mganga mkuu wa Manispaa Charles Mkombachepa alisema kituo hicho cha afya cha kisasa kina majengo hayo 10 ya kutolea huduma ambayo ni jengo la wagonjwa wa nje (OPD), jengo la akina mama wajawazito, jengo la maabara ,jengo la upasuaji akina mama wajawazito, jengo la akina mama wajawazito wanaojifungua na wenye shida mbalimbali za uzazi .
Mganga mkuu wa Manispaa pia alisema kituo hicho cha afya kina nyumba moja ya mtumishi , jengo la kufulia nguo pamoja na jengo la kuhifadhia maiti.

Nao wakazi wa Kata hiyo akiwemo Leticia Lukanima ameipongeza Manispaa kwa kujenga kwanza Zahanati katika eneo hilo inayowasidia kupata huduma za afya wakiwa karibu tofauti na miaka ya nyuma wakizifuata umbali wa kilometa tano kwenye kata nyingine ya Kichangani kabla ya kuanza mradi huo mkubwa wa kituo cha afya.

“ Tunampongeza Rais wetu kwa kutusogezea huduma hapa Tungi , tunapata huduma nzuri kutoka kwa wauguzi na madaktari na tunaangalia majengo mengine yanayojengwa ya kituo cha afya kikikamilika kitaboresha huduma zaidi na kutuondolea kufuata vipimo vya afya vituo vya mbali “ alisema Leticia



Picha mbalimbali za matukio ya siku ya Lishe Duniani, Kata ya Mafiga















# Muonekano wa Shule Mpya ya Sekondari Lukobe



# MANISPAA MORO YAJENGA SHULE YA SEKONDARI MPYA YA GHOROFA MBILI KWA FEDHA ZA MAPATO YA NDANI.



Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imepanga kutumia kiasi cha Sh bilioni 1.1 kwa ujenzi wa Sekondari maalumu ya ghorafa mbili katika kata ya Boma kwa kutumia fedha za mapato ya ndani.

Shule hiyo mpya ya ghorofa mbili ikiwa na vyumba vya madarasa 15, ofisi za walimu pamoja na mkuu wa shule imeanza kujengwa kuanzia mwaka wa fedha wa 2021/2022 katika kata hiyo kutokana na kuwa eneo dogo la ardhi na hadi sasa zimetumika Sh milioni 650 kwenye ujenzi huo.

Mkurugenzi wa Manispaa Ndg. Ally Machela alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea kuona miradi ya sekta ya elimu inayotekelezwa na kusimamiwa na Manispaa ukiwemo ujenzi wa shule mpya ya ghorafa mbili

" Mradi huu unakisiwa kutumia kati ya Tsh milioni 800 hadi Tsh bilioni 1.1 hadi utakapokamilika na hivi sasa umeshatumia kiasi cha Sh milioni 650 hadi ulipofikia ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa " alisema Machela

Alisema kwa sasa ujenzi umefikia hatua ya upauaji na ujenzi wake unatarajia kukamilika mwaka huu wa fedha wa 2022/2023 kwa asilimia 100 na kuwezesha wanafunzi wa kata hiyo ifikapo Januari , 2023 kuwa madarasani.

"Tumepata mawazo mbalimbali ya wadau wakishauri iwe sekondari maalumu kwa ajili ya watoto wa kike na wengine kushauri iwe ni sekondari maalumu ya mchepuo wa masomo ya sayansi " alisema Machela

Mbali na fedha za mapato ya ndani alisema , Manispaa yenye kata 29 bado nyingine hazina shule za sekondari ,lakini mwaka uliopita zimejengwa shule mpya nne kwa gharama ya Sh Bilioni 1.7 .

Machela alisema shule hizo zimejengwa kutokana na fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya Covid – 19.

" Shule hizi mpya tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha za madarasa 86, lakini katika madarasa 40 tuliamua kuanzisha shule mpya kwa maana ya sekondari mpya katika kata ya Mbuyuni, Tungi , Mkundi na Mazimbu na tayari zimesajiliwa na wanafunzi wa kidato cha kwanza wameanza masomo" alisema Machela

Katika hatua nyingine alisema , Manispaa ilipokea fedha Sh milioni 940 kati ya Bilioni 1.2 kutoka Serikali kuu kupitia Mradi wa Kuboresha Mazingira ya Kufundishia na Kujifunzia kwa Elimu ya Sekondari (SEQUIP).

Alisema fedha hizo zimetumika kwa kujengwa shule mbili mpya za sekondari katika kata ya Mindu na Lukobe na kila moja ilipewa Sh Milioni 470 ambapo vyumba 16 vya madarasa yamekamilika.

Machela alisema ,ujenzi huo umehusisha maabara sita , maktaba mbili , vyumba vya Tehama ,majengo mawili ya utawala na matundu 40 ya vyoo na kwamba majengo hayo

yamepauliwa na kuezekwa , kupingwa rangi na hatua nyingine za umaliziaji.
Kwa uande wake Meya wa Manispaa hiyo , Pascal Kihanga alisema kwa mwaka wa fedha 2022/23 imepanga kukamilisha miradi ya maendeleo na kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Naye Ofisa Taaluma Sekondari wa Manispaa hiyo, Herieth Kagosi alisema uboreshwaji wa miundombinu ya elimu na ujenzi wa shule mpya kunaifanya Manispaa kujipanga kuboresha taaluma ya elimu na kufuta ziro katika shule zake 27 za sekondari zilizopo .
Kwa upande wake Mwenyekiti wa mtaa wa Mindu Shomari Ahuman alisema baada ya kujengwa kwa shule ya sekondari katika kata yao , wananchi wamejipanga kushiriki kikamilifu kusaidia ujenzi wa nyumba za walimu baada ya serikali kuu kutoa fedha .

# Vijana tumieni fursa ya uwezeshaji wa Mikopo inayotolewa na Halmashauri kujikwamua kiuchumi.

Watanzania wakiwemo vijana nchini wameshauriwa kuchangamkia fursa za uwezeshaji wa mikopo inayotolewa na Serikali kupitia Halmashauri za wilaya , Manispaa na Majiji ili waanzishe miradi ya ujasiliamali ya kujikwamua na umaskini wa kipato.
Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2022 , Sahil Geraruma alitoa rai hiyo katika Kata ya Mazimbu Manispaa ya Morogoro baada ya Mwenge wa Uhuru kupitia kuona mradi wa kikundi cha vijana wa Chama cha Mafundi Ujenzi.

Geraruma alisema , Serikali ya awamu ya sita inawajali wananchi wake kwa kutoa fursa mbalimbali zikiwemo za mikopo isiyo na riba kwa makundi ya vijana , wanawake na watu wenye ulemavu kupitia fedha zinazotolewa na Halmashauri za wilaya, Manispaa na Majiji.

“ Kwanza kabisa naomba niwafikishie habari njema vijana , kuna asilimia 10 zinazotokana na makusanyo ya fedha za ndani za Halmashauri na asilimia hiyo imegawanyika katika makundi matatu asilimia nne ni kwa vijana umri kuanzia miaka 18 hadi 35 “ alisema Geraruma

Alisema wanachopaswa ni kufuata utaratibu wa kuunda vikundi , kusajili kikundi , kuunda katiba ya kikundi kwa kuzingatia sheria ndogo ndani ya Halmashauri husika , kufuata taratibu zote kwenye Ofisi ya Maendeleo ya Jamii na ya Mkurugenzi mtendaji na mkopo huo hauna riba.
Geraruma alitaja kundi lingine la wanawake ambalo lina asilimia nne na kwamba utaratibu ni kuunda vikundi vya watu kuanzia watano na sheria inataka wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea.
Kundi lingine linalonufaika na mkopo huo ni la watu wenye ulemavu ambalo limetengewa asilimia mbili pia kwa utaratibu wa kuunda vikundi lakini wao hata mtu mmoja mmoja anaweza kukopeshwa.

“ Kwa hiyo ndugu zangu Rais ametoa fursa tunaweza kunufaika nayo , watanzania wenzangu zingatieni fursa hiyo ili tuweze kunufaika , tusikae mitaani tukaanza kulalamika kila wakati maisha magumu. Wakati kuna fursa Rais ametoa na hatujazitumia “ alisema Geraruma
Aliwataka vijana kuchangamkia fursa hiyo kwa kufuata utaratibu uliowekwa kupata mikopo isiyo na riba ili iwawezeshe kuanzisha shughuli mbalimbali za kiuchumi ambazo zitawasaidia kuboresha maisha yao na pia kukuza uchumi wa Taifa .

Pamoja na hayo aliwataka wanufaika na mikopo hiyo kurejesha kwa wakati ili iendelee kutolewa kwa wenzao wengine na endapo kutajitokeza changamoto za kuchelewa kurejesha wanapaswa kuwasiliana na viongozi wa ngazi ya Halmashauri kutatua changamoto zilizopo.
Geraruma pia alitumia fursa hiyo kuipongeza Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kupitia Mkurugenzi wake kutenga fedha za asilimia 10 zitokanazo na mapato ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo kwa makundi ya wanawake , vijana na watu wenye ulemavu.

Awali Katibu wa Kikundi cha vijana wa Chama cha Mafunzi Ujenzi , Annastazia Charles akitoa taarifa ya mradi huo kwa Kiongozi wa mbio cha Mwenge wa Uhuru alisema kikundi kilianzishwa mwaka 2018 kikiwa na wanachama 11 ambapo wavulana ni tisa na wasichana wawili na kilipata usajili wa Manispaa mwaka 2020.
“ Kikundi hiki kinajishughulisha na kufyatua matofali mchanganyiko wa saruji na mchanga (blocks) kwa kutumia mtambo wa kushindilia mchanga na saruji” alisema Annastazia

Alisema mwaka 2021/2022 kikundi kilipata mkopo wa Sh milioni 24 ikiwa ni sehemu ya mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Manispaa kwa makundi ya ( wanawake, vijana na watu wenye ulemavu )na fedha hizo zilitumika kununua mashine mbalimbali na vifaa vya kufyatua matofali katika mradi huo .

Annastazia alisema hadi sasa mradi huo una thamani ya Sh milioni 39.2 ambazo Tsh milioni 24 ni mkopo kutoka Halmashauri ya Manispaa na Tsh Milioni 15.2 ni mchango wa wanachama ukiwa ni mtaji wa kikundi chenyewe na mradi umekamilika na unatoa huduma.




JIWE LA MSINGI LA UJENZI WA
KITUO CHA AFYA LUKOBE
LIMEWEKWA NA KIONGOZI WA
MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA
NDG. SAHILI NYANZABARA GERARUMA
TAREHE 28.08.2022





Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini Mhe. Abdulaziz Abood (atikati) akizungumza na wananchi wa Lukobe katika uwekaji wa jiwe la Msingi kituo cha Afya Lukobe wakati wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Agosti 2022

## MBUNGE WA JIMBO LA MOROGORO MJINI MH. MOHAMMED AZIZ ABOOD AMETOA AHADI YA GARI LA WAGONJWA (AMBULANCE)

Mhe.Abood ametoa ahadi hiyo Agosti, 28/2022 katika Mbio za Mwenge wa Uhuru ulioweka jiwe la Msingi kituo cha afya cha Lukobe.

Mhe.Mbuge amesema mara baada ya ujenzi kukamilika, atatoa gari la wagonjwa moja, ambalo mpaka sasa likotayari, Gari hilo litatumika na wananchi wa Lukobe, ili kusaidia wagonjwa wote hasa katika kuokoa maisha ya wakina mama wajawazito na watoto.

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Ndugu, Sahili Geraruma amempongeza sana Mhe. Mbunge kwa kuwa na upendo kwa wananchi wake na kuwa Mbunge ambaye anajua kutumia uongozi wake, maana kiongozi Bora ni yule anayejua kunyanyua wananchi wake pale ambapo wameshindwa kuendeleza.

Aidha Mhe. Abood amewaomba wananchi kuendelea kuwa na subira na kuwa waadilifu na kutunza kituo hicho ili kiweze kutumika na vizazi vingine.

## MADIWANI WAFURAHISHWA NA KAZI ZA WAJASILIAMALI.

Madiwani wa Manispaa ya Morogoro wametembelea maonyesho ya nane nane Agosti 8,2022 kwa ajili ya kujifunza teknolojia mbalimbali mpya za Kilimo, Mifugo na Uvuvi na kutembelea Banda na vipando vya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro katika uwanja wa Mwalimu Julius Nyerere.

Ikiwa ndio siku ya mwisho ya maonyesho ya nane nane ya Kanda ya Mashariki, Waheshimiwa Madiwani wakizunguka katika mabanda na vipando vya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro wamevutiwa na kazi nzuri za wajasiliamali hasa kwenye ubunifu wa kufuga samaki na kulima mboga za majani kwa kutumia maji ya kufugia samaki.

Ubunifu huo unaweza kuotesha mboga bila kutumia mchanga na mbolea yeyote kwasababu maji hayo ya kufugia samaki yanakuwa na virutubisho vya kutosha vinavyowezesha kuotesha mmea bila changamoto yeyote.

Pia Waheshimiwa Madiwani wamefurahishwa sana na Lishe Tiba, wajasiliamali wengine wamejikita kutafuta tiba za magonjwa mbalimbali kupitia mimea au mchanganyo wa nafaka mbalimbali, jambo ambalo ni la kuwahakikishia wa Tanzania kuwa na Afya Bora na kufuta utapia mlo.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro ametoa shukrani za dhati kwa Wajasiliamali wote kwa kushiriki nasi katika maonyesho hayo na kuwaomba kujipanga kimalifu katika maonyesho ya jayo.

**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa
Tanzania





Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogro Ally Machela akimkabidhi funguo za gari Mratibu wa TASAF Felician Katemana kwa ajili ya kurahisisha shughuli mbalimbali zinazotekelezwa naKitengo hicho cha TASAF



# MANISPAA YA MOROGORO YATOA SHUKRANI KWA RAIS SAMIA KUPATIWA GARI LA TASAF.

- **Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro yampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa Uongozi bora**

MANISPAA ya Morogoro, imetoa shukrani za pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hasssan, kutona na kukabidhiwa gari mpya itakayotumiwa na Ofisi ya TASAF.

Pongezi hizo, zimetolewa na Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Ally Machela, julai 10/2022 katika hafla fupi ya kukabidhi gari hilo kwa Maratibu wa TASAF Manispaa ya Morogoro. Machela,amesema kuwa  agari hilo limekabidhiwa kwa ajili ya utekelezaji kwa shughuli za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

“Tumepokea gari hili likiwa limekamilika kila kitu, utunzaji ni muhimu sana, lakini sikatai kutumika katika shughuli nyengine, yaweza kutumika kwenye shughuli nyingine za Halmashauri pale kunapokuwa na shughuli nyingine za kiujumla  lakini kipaumbele ni shughuli za TASAF, isitokee shughuli za TASAF zikashindwa kufanyika kwa kukosekana usafiri ni wajibu wa Afisa usafirishaji na dereva wa gari hili kuwa na mawasiliano ya kina na Ofisi ya TASAF kama kuna shughuli nyingine zinahitaji kufanyika kwa kutumia gari hilo”Amesema Machela.

Naye Maratibu wa TASAF Manispaa ya Morogoro, Feliciana Katemana, amesema gari hilo watalitunza na litatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

ikumbukwe kuwa Rais Samia alifanya hafla hiyo ya kukabidhi magari ya TASAF  katika Viwanja vya Posta, Kijitonyama Jijini Dar es Salaam tarehe 01 Juni, 2022 ambapo jumla ya magari 241 yamekabidhiwa kwa Halmshauri ikiwa ni njia ya kuimarisha shughuli za utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO
OFISI YA MKURUGENZI
S.L.P 166
MOROGORO TANZANIA

(C) 2020